# BRIGHT VISION SERIES

## DARASA LA NANE - MWAKA - 2023

## KISWAHILI : LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu sahihi kujazia pengo.***

Kabla ya kengele kugongwa wakati __1__ tulikuwa __2__ mchezo wetu tulioupenda wa kujificha na kutafutana yaani__3__. __4__, tulisikia mlipuko wa __5__ uliotuacha __6__ wazi tusijue la kutenda. __7__ tulichana mbuga tusijue tuelekeako. Kila mtu njia yake. Kufumba na kufumbua, nilijikuta __8__ mwa mwalimu. Mvua kubwa ilifuatia baadaye.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. uo | B. huu | C. huo | D. hii |
| 2. | A. tunacheza | B. tukicheza | C. tumecheza | D.tunachezacheza |
| 3. | A. natiki | B. kibunzi | C. foliti | D. kibe |
| 4. | A. Gafla bin vuu | B. Gafla bin vu | C. Ghafla bin vu | D. Ghafla bin vuu |
| 5. | A. radi | B. risasi | C. mdomo | D. bomu |
| 6. | A. vinywa | B. kinywa | C. mdomo | D. maneno |
| 7. | A. wote | B. nyote | C. sote | D. yote |
| 8. | A. afisi | B. afisini | C. katika afisini | D. kwa afisi |

Sigara imewafanya vijana kudhoofisha afya __9__ pamoja na dawa __10__kulevya __11__ __12__ vingi vya uhalifu __13__ vijana hawa. Ni jukumu letu sote kusitisha ulaguzi wa dawa__14__ ili zisiathiri jamii tena. Tukumbuke kuwa umoja ni nguvu__15__ ni udhaifu.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. zao | B. yao | C. yenu | D. zenu |
| 10. | A. zingeneza za | B. nyinginezo za | C. zingenezo za | D. mengine ya |
| 11. | A. zimesababisha | B. yamesababisha | C. imesababisha | D. itasababisha |
| 12. | A. viza | B. visa | C. vihoja | D. vioja |
| 13. | A. miongoni ya | B. kati ya | C. baina za | D. katikati ya |
| 14. | A. hizi | B. hii | C. hi | D. zile |
| 15. | A. vitendo | B. utangamano | C. utengamano | D. utengano |

**Kutoka swali 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa.**

16. Akisami hii $^4/_7$ huitwa
    A. nne kwa saba B. subui nne
    C. robo saba D. sudusi nne
17. Ni nini wingi wa sentensi ifuatayo?
    **Mtoto wangu amefuzu vizuri.**
    A. Watoto wangu wamefuzu vizuri.
    B. Watoto wao wamefuzu vizuri.
    C. Watoto wetu wamefuzu vizuri.
    D. Watoto wenu wamefuzu vizuri.
18. Kukanusha kwa
    **Chungu kilichonunuliwa kiliuzwa tena.**
    A. Chungu kilichonunuliwa hakijauzwa tena.
    B. Chungu kiliyonunuliwa hakikuuzwa tena.
    C. Chungu kisichonunuliwa hakijauzwa tena.
    D. Chungu kisichonunuliwa kiliuzwa tena.
19. Chagua kinyume cha sentensi ifuatayo.
    **Jana jioni niliondoka.**
    A. Jana asubuhi niliondoka.
    B. Jana jioni nilirudi.
    C. Kesho asubuhi nitarudi.
    D. Kesho jioni nitaondoka.
20. Tumia kiashiria kisisitizi kifaacho.
    **Mimi ninaitaka chai __________**
    A. hizi hizi B. uu huu
    C. hii hii D. ii hii
21. Tegua kitendawili: **Nyama nje ngozi ndani.**
    A. nyuki B. firigisi
    C. mkebe D. ulimi
22. Mtu ambaye anapenda nchi yake na yu tayari kuifia ni
    A. mzalendo B. raia
    C. balozi D. mwananchi

23. Chagua jibu la viarifu pekee
   A. gunia, bawaba, mchi
   B. papa, baba, dada
   C. kata, cheza, uma
   D. mwerevu, mdogo, mfupi

24. Taja jina la umbo hili



   A. mstari sulubu  B. geli
   C. wimbi  D. mstari sambamba

25. Kivumishi katika sentensi hii ni:
   **Wachezaji wanne walipewa zawadi.**
   A. walipewa  B. wachezaji
   C. zawadi  D. wanne

26. Ni sentensi ipi sahihi:
   A. Niliingia kwa nyumba.
   B. Niliingia katika nyumbani.
   C. Niliingia nyumbani.
   D. Niliingia ndani ya nyumbani.

27. Dada wa mama ni:
   A. shangazi  B. mjomba
   C. ami  D. hale

28. Taja kiwakilishi katika sentensi.
   **Wote watiifu walipokea zawadi zao jana.**
   A. wote  B. watiifu
   C. zao  D. jana

29. Mwana wa simba hitwa
   A. kiyoyo  B. shibli
   C. kinegwe  D. kisuse

30. Neno <u>kuwalaumu</u> lina sialbi ngapi?
   A. 6  B. 5
   C. 9  D. 10

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.</u>**

Sisi vijana inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu tuweze kupata ufanisi na uwezekano na kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi ni nyumba ya njaa." Kwa hivyo, basi haifai **kulaza damu.** Ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja.

Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani nchini mwetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwa bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, maadamu kila uchao idadi ya adinasi inaongezeka.Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula.

Zaidi ya hayo, lazima pia tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatubidi tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni na hata katika jamii lazima yatusaidie kutambua mbinu za kufanikiwa. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itatufanya kujua wajibu wetu katika jamii na kutufanya tuone mbele. Sisi vijana kukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu lazima washirikiane na kufikira kwamba wao ni wamoja. "Utengano ni udhaifu. "Lugha ya taifa ndiyo chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu, wakati tunapokosea lazima tukubali tumekosea na kufanya masahihisho mara moja. Tusikasirke kwa sababu tumesahihiswa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi pia kutafuta njia za kuyatatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana tunashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani kwetu. Ili adinasi wamudu kuishi ausi bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo.

Tukiwa na viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki kuwa mikia siku zote. Bahati mbaya ni kuwa wananchi wengi siku hizi kuchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama utajiri wake. Kwa hivyo basi, tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba kubwa au ya utajiri.

31. Mambo mawili wanayozingatia vijana kazini kulingana na aya ya kwanza ni
   A. bidii na ari
   B. bidii na uvumilivu
   C. ari na uaminifu
   D. imani na ari
32. Maana ya msemo **kulaza damu** ni
   A. kukawia katika utendaji
   B. kunyamazia tatizo
   C. kulala kazini
   D. kukosa makini
33. Elimu ya vijana na watu wazima inatiliwa mkazo ili
   A. kuongeza busara, adabu na jitihada
   B. kuimarisha mipango ya kujistawisha
   C. kuzidisha kiwango cha mazao mashambani
   D. vijana waweze kuajiriwa sahihi
34. Tambua maelezo yaliyo sahihi
   A. wananchi wengi wamejishughulisha katika biashara.
   B. wananchi wametambua umuhimu wa watu.
   C. matatizo ya nchi huletwa na wingi wa watu.
   D. wengi hujishughulisha na elimu ili wapate kazi.
35. Mtazamo wa mwandishi ni kuwa elimu inayotolewa
   A. ni duni
   B. inafaa sana
   C. inawafaa vijana tu
   D. ni ya wote
36. Vijana katika aya ya nne wanahimizwa
   A. wawe mfano bora kwa wengine.
   B. wakumbatie elimu inayotolewa.
   C. wawanie uongozi siku za baadaye.
   D. watetee kubadilishiwa mfumo wa elimu.
37. Jukumu ya lugha ya taifa kwa mujibu wa makala haya ni
   A. kuinua viwango vya elimu, kuwasilisha mapendekezo.
   B. kupitisha utamaduni, kuzorotesha ushirikiano.
   C. kuziunganisha jamii kupitisha hisia za watu.
   D. kuwaunganisha watu, kutolea mafunzo mbalimbali.
38. **Tunapokosea lazima tukubali.** Ni methali ipi inayoweza kuelezea vizuri kifungu hiki?
   A. Ukisutwa sukutua
   B. Kweli ndiyo fimbo ya kukamata
   C. Usipoziba ufa utajenga ukuta
   D. Mchelea haki hatendi ukweli
39. Kiongozi mzuri ni yule ambaye
   A. huyaweka maslahi yake mbele ya wengine.
   B. huwajibikia ufanisi wa taifa lote.
   C. hupinga maovu mengi kwa maneno makali.
   D. hupendwa na watu wote kwa ukwasi alio nao.
40. Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni:
   A. Jukumu la vijana wazalendo.
   B. Umuhimu wa mfumo bora wa elimu
   C. Manufaa ya kuwa na viongozi waaminifu
   D. Umuhimu wa vijana nchini

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.**

Nilipoabiri matwana kuelekea kwetu mashambani, nilikuwa na **shauku** kubwa ya kuwaona watu wa mlango wangu. Nilitamani kupata kilalio kilichotayarishwa na mke wangu. Vilevile nilitarajia kuchezacheza na kumhadithia mwanangu Nyoni jioni hiyo. Hata hivyo, hayo hayakutimia kwani safari yetu ilienda shoto punde tu tulipopita mji wa Thika.

Tulikuwa tumesafiri kwa **takribani** robo tatu ya saa kutoka Nairobi. Ninakumbuka vyema kabisa kuwa ulikuwa mwendo wa saa mbili usiku. Mvua ilikuwa ikinyesha **kidindia.** Mara, kufumba na kufumbua msafiri mmoja aliyekuwa ameketi ubavuni mwa **mshika usukani** alitoa bastola. Kwa sauti ya radi, alimwamuru dereva alielekeze gari kwenye njia iliyoelekea katika shamba la mibuni lililopakana na mashamba ya minanasi.

Lo! Dereva hakuwa na jingine ila kusalimu amri kwani lisilo budi hubidi. Kimya kilitawala mle garini. Kicheko cha bashasha na mazungumzo baina ya abiria yalikatika ghafla. Tulifanya matumbo moto. Nyoyo zilitupapa tulipong'amua kuwa tayari tulikuwa mikononi mwa watekanyara.

Baada ya kusafiri kwa mwendo wa kilomita mbili hivi, dereva aliamrishwa aliegeshe gari. Kote kulikuwa kimya isipokuwa sauti ya matone ya mvua na ngurumo za radi za mara kwa mara. Giza lilikuwa totoro ila mwanga wa umeme uliokuwa ukitupofua macho mara kwa mara. Giza lilikuwa totoro ila mwanga wa umeme uliokuwa ukitupofua macho mara kwa mara. Tayari, wengi wetu tulikuwa hatujiwezi kwa woga. Bila kujali mvua, majambazi hao walituamrisha tutoke nje ya gari pasipo kuchukua chochote. Pindi tulipotoka, majambazi wale walitupofua macho kwa kurunzi walizokuwa nazo. Hakuna aliyeamini sikio lake tulipoamrishwa tuvue

nguo zote. Lo! Yapi haya? Mzee mmoja aligongwa kinywani na kuyatema meno kadhaa alipoapa kwamba hata kwa mtutu wa bunduki, asingevua nguo zake mbele ya mkazamwana wake.

Tulipoona hayo, tulishika roho mikononi. Dakika tano baadaye, sote tulikuwa uchi wa mnyama. Mabaradhuli wale walizisheheni mali zetu garini na kuondoka. Tuliachwa hapo tukiwa na wasiwasi na woga huku tumechanganyikiwa tusijue la kufanya. Tulikuwa kama vifaranga mama yao achukuliwapo na mwewe.

Baada ya kuwaza na kuwazua kwa muda, mzee mmoja alisema tupige kamsa kwa pamoja ili iwapo palikuwa na waja hapo karibu waje watusaidie. Wazo hilo tuliliona kuwa tasa na kulitupilia mbali. Badala yake, tuliamua kuchapa miguu hadi katika gurufu ili kuomba usaidizi.

Hata baada ya kufika gurufuni, mambo yalizidi kutuendea upogo kwani tulipojaribu kuwapungia madereva mikono, walitudhania kuwa ni majini na kuongeza mwendo. Mambo yalipozidi kutokota, nilikata kauli kushika njia hadi kiamboni. Niliwasili nyumbani mwendo wa majogoo nikiwa hoi kwa kutembea huku nikitetemeka kama unyasi nyikani wakati wa upepo. Nusura mke wangu Rosa azimie aliponiona. Lo! Si aibu hiyo. Lakini ningefanyaje? Mungu waokoe wezi wabadilike. Wawe watu wema duniani.

41. Msimulizi alikuwa
  A. na hamu ya kufika kwake.
  B. akiwatolea wenzake hadithi.
  C. na shauku ya kuuona mlango wa nyumba yake.
  D. na tamaa ya kula kiapo.

42. Kwa nini safari ya wahusika ilitumbukia nyongo?
  A. Walipata ajali
  B. Gari lilipata hitilafu
  C. Walinaswa na majambazi
  D. Walipokonywa mali zao

43. Yaelekea wahusika waling'oa nanga kwa safari yao lini?
  A. Wakati wa mvua
  B. Saa tatu kasorobo usiku
  C. Saa moja na robo jioni
  D. Majogoo

44. Mhalifu aliyekuwa na bastola alikuwa wapi?
  A. Aliketi sako kwa bako na dereva.
  B. Alikuwa nje ya gari.
  C. Alikuwa mbele ya gari.
  D. Alikuwa gurufuni.

45. Kwa nini mazungumzo ya abiria yalikatika ghafla?
  A. Waliamriwa wanyamaze
  B. Walishtuliwa na mfyatuko wa bunduki
  C. Waliogopa kuonekana na watekanyara
  D. Walihofia maisha yao

46. Gari lilisafiri kwa masafa yapi likiwa mikononi mwa majambazi?
  A. Mita elfu mbili
  B. Mita mia mbili
  C. Kilomita moja
  D. Mita chache

47. Gari husika uulekezwa katika shamba la zao lipi?
  A. Mananasi
  B. Kahawa
  C. Maparachichi
  D. Miwa

48. Mwangaza wa mara kwa mara ulitokana na nini?
  A. Kurunzi
  B. Radi
  C. Umeme
  D. Nyota

49. Walipokosa usaidizi wahasiriwa walifanya nini?
  A. walienda nyumbani mwao
  B. walipiga unyende
  C. walienda kituoni pa polisi
  D. haijabainika

50. Methali ipi ambayo si mwafaka kutumiwa kuelezea makala haya?
  A. Dunia ni mwendo wa ngisi
  B. Siku za mwizi ni arubaini
  C. Usikate mbeleko kabla mwana hajazaliwa
  D. Ibilisi wa mtu ni mtu